

# StEPS

Uchunguzi wa Kuona kwa  
Watoto kabla kwenda  
shuleni Jimbo zima

Statewide Eyesight Preschooler Screening



**Habari za mawasiliano  
ya Huduma ya Afya ya Mtoto  
na Familia**



Nini unachohitaji kujua kuhusu  
mpango wa StEPS

## StEPS ni nini?

Mpango wa StEPS imeanzishwa na Wizara ya Afya NSW na inatoa uchunguzi bure wa kuona kwa watoto wote wa umri wa miaka 4.

## Kwa nini mtoto wangu anahitaji kuchunguzwa kuona kwake?

- Watoto wanalalamika mara chache kuhusu matatizo ya macho
- Watoto wanaweza kutotambua hawaoni vizuri
- Watoto wengine wanaweza kuona vizuri na jicho moja lakini wanaweza kupata shida ya kuona na jicho lingine
- Macho ya watoto wanaweza kuonekana vizuri na wazazi/walezi wanaweza kufikiri kwamba mtoto wao anaona vizuri lakini bado watoto wengine wanaweza kuwa na tatizo la kuona bado
- Njia pekee kufahamu kama mtoto ana tatizo la kuona ni kupima kuona kwa mtoto jicho moja ndipo jicho lingine.



## Je, ulijua hii?

- Kama mtoto ana 'jicho la uvivu' linaweza kusababisha kupotea kwa ukali kwa kuona au upofu katika jicho lile kama halitibwi
- Kama mtoto ana tatizo la kuona, mapema zaidi yawezekanayo tatizo litagunduliwa na kutibwa yaani matokeo ya kuona yatakuwa nzuri zaidi
- Kama wazazi walivaa miwani au walikuwa na matatizo ya kuona walipokuwa mtoto, basi watoto wao wanawezakana zaidi kuwa na matatizo ya kuona pia
- Baada ya umri wa miaka minane matatizo mengine ya kuona kwa utoto hayawezi kutibwa na mtoto atakuwa na matatizo ya kuona kwake kwa iliyobaki ya masiha yake – hata miwani haitasaidii
- Watoto wachanga wenye uzito mdogo wa kuzaliwa na watoto wenye matatizo ya nyurolojia wana hatari zaidi kuwa na matatizo ya macho

## Je, mtoto wangu anahitaji kuchunguzwa kuona kwake?

Afya NSW inashauri watoto wote kuchunguzwa kwa kuona kwao kabla ya kuanza kwenda shuleni na inashauri na nguvu kwa watoto wote wenye umri wa miaka 4 kushiriki katika mpango wa uchunguzi wa kuona.

## Je, mtoto wangu anawezaje kufikia mpango wa StEPS?

Mkoa wa Afya wa Eneo lako utalenga mashule ya chekachea na vituo vya utunzaji wa watoto kutoa uchunguzi **bure** wa kuona kwa watoto wote wa umri wa miaka minne. Ili kuchunguza kuona kwa mtoto wako utahitaji kujaza fomu ya kukubali na kuirudisha kwa kituo cha shule la kuchekachea/ kituo cha utunzaji wa watoto. Unaweza kupanga uchunguzi wa kuona kwa mtoto wako wa umri wa miaka minne **bure** kupitia Huduma ya Afya ya Mtoto na Familia ya eneo lako. Habari za mawasiliano kwa Huduma ya Afya ya Mtoto na Familia ya eneo lako zipo upande mwingine ya broshua hii.



## Nitajuaje kama mtoto wangu ana tatizo la kuona?

Kila mzazi/mlezi wa watoto wanao uchunguzi wa kuona atajulishwa matokeo ya kadirio ya uchunguzi wa kuona kwa mtoto wao. Kama tatizo la kuona likigunduliwa utawasiliana na Mkoa wa Afya ya Eneo lako na kuombwa kupanga macho ya mtoto wako kupimwa kabisa na bingwa wa afya ya macho.

Kwa sababu macho ya watoto yanaendelea kua mpaka karibia umri wa miaka 8 ni muhimu kuhakikisha kuona kwa kila mtoto kunaendeleza kwa kawaida katika miaka hiyo ya kua.

Mpango wa StEPS ni mpango wa uchunguzi wa kuona na haitoi kadirio ya utambuzi mzima. Kama una mashaka kuhusu kuona kwake kwa mtoto wako, unapendekezwa kupanga kwa kuona kwa mtoto wako kupimwa kabisa na bingwa wa afya ya macho.